# MFUKO WA MAENDELEO YA ZAO LA KAHAWA TANZANIA-TCDF

## RIPOTI YA UENDESHAJI YA MWAKA 2014/15

## NCC TAREHE 26-27 Mei 2016

## Nashera Hotel,Morogoro,

# 1.0.UTANGULIZI

Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Kahawa Tanzania (TCDF) ulianzishwa Mwaka 2011 katika Mkutano Mkuu wa mwaka wa Wadau uliofanyika Mjini Morogoro. Mfuko ulisajiliwa na kuanza rasmi Mwaka 2012 .

Kwa mujibu wa makubaliano ya Wadau, Wadau wanachangia fedha za kugharamia utekelezaji wa majukumu ya pamoja na shughuli za uendelezaji wa zao la kahawa kama ifuatavyo:

1. 0.75% kwa ajili ya utafiti na uzalishaji wa miche (TaCRI)
2. 0.2% kwa ajili ya uendeshaji wa minada (TCB)
3. 0.2% kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi ya Mfuko.

# 2.0. UTEKELEZAJI WA MALENGO

Kwa mwaka 2015/2016 Mfuko ulipanga malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa mpango wa kugharamia upatikanaji wa pembejeo hususan mbolea kwa wakulima wa kahawa
ii. Kuimarisha menejimenti na uendeshaji wa Mfuko; na
iii. Kuongeza uwezo wa kifedha wa Mfuko kwa lengo la kuimarisha ugharamiaji wa maendeleo ya zao la kahawa.

# 2.0 **UTEKELEZAJI WA MALENGO**

Kwa kuzingatia malengo tajwa hapo juu, Mfuko umefanya yafuatayo:-

1. **Mpango wa ugharamiaji upatikanaji wa pembejeo.**

- Mfuko kupitia Mtaalamu mwelekezi umekamilisha kuanda andiko la Mpango wa kugharamia upatikanaji wa pembejeo hususan mbolea kwa wakulima wa kahawa.

- Tayari andiko limewasilishwa katika Mkutano huu na wadau wametoa maoni na mapendekezo ambayo yatazingatiwa katika kuboresha andiko husika na utekelezaji wa Mpango tajwa.

- Hivyo Mfuko unaomba idhini ya wadau ili uweze kuendelea na Mpango huo kwa mwaka 2016/2017

# 2.0 **UTEKELEZAJI WA MALENGO**

## 2 Kuimarisha menejimenti na uendeshaji wa Mfuko

- Mfuko utaendelea na ajira za watendaji wa Mfuko kadiri uwezo utakavyoruhusu na mahitaji ya nafasi husika.
- Mfuko unaendelea pia kuandaa na kuboresha nyaraka mbalimbali za uendeshaji Mfuko kwa kuzingatia sheria na kutekeleza dhana ya uwazi na utawala bora.
- Hivyo Mfuko unaomba wadau kuendelea kutoa ushirikiano kwa wadau katika kuimarisha menejiment na uendeshaji wa shughuli za Mfuko

# 2.0 Utekelezaji wa Malengo

**3 Kuongeza uwezo wa kifedha wa Mfuko kwa lengo la kuimarisha ugharamiaji wa maendeleo ya zao la kahawa**.

- Mfuko umekuwa ukichukua hatua mbalimbali kwa lengo la kuongeza uwezo wa kifedha wa Mfuko. Miongoni mwa hatua hizo ni pamajo na:-
  - Kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo vingine vya fedha mbali na michango wa wadau;
  - Kuendelea kufuatilia utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kuchangia fedha katika Mfuko; na
  - Kuiomba Serikali kupunguza baadhi ya makato na tozo katika zao la kahawa ili wadau waweze kuchangia shughuli za Mfuko
- Hivyo, kupitia nafasi hii, tunaomba Serikali itekeleza ahadi yake ya kuchangia Mfuko na kuwezesha ugharamiaji wa shughuli za maendeleo ya tasnia ya kahawa

# 2.3 Changamoto za Mfuko

Pamoja na kutekeleza malengo ya Mfuko kwa kiwango tajwa hapo juu, Mfuko unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Ufinyu wa bajeti ya Mfuko unaosababishwa na wadau kushindwa kuchangia fedha kuendana na mahitaji ya Mfuko;
- Uwepo wa makato na tozo nyingi katika tasnia ya kahawa hususan kwa wakulima; na
- Serikali kutotekeleza ahadi yake ya kuchangia fedha katika Mfuko.

# 3.0.TAARIFA FUPI YA FEDHA

Michango kwa ajili ya shughuli shirikishi

i. Utafiti (TaCRI): 1,728,570,117/-
ii. Uendeshaji wa Minada(TCB):463,777,949/-
iii. Uendeshaji wa ofisi ya Mfuko: 461,939,126/-

Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu kwa Mwaka ulioisha tarehe 30.6.2015 ulifanywa na Wakaguzi wa Mfuko ambao ni M/S Mikimas Associates.

# 3.0.TAARIFA FUPI YA FEDHA

**3.1** Kuwasilisha Hati ya Maoni ya Ukaguzi (Opinion)

a) Misingi ya ukaguzi ilitekelezwa kwa viwango vya kimataifa. (International Standards on Auditing – ISA)
b) Wakaguzi walipewa vielelezo na nyaraka kwa kadri walivyohitaji kwa ajili ya ukaguzi.
c) Mahesabu yanakubaliana na vitabu
d) Hati safi ambayo haina dosari ilitolewa kwa Mfuko.

# TAARIFA FUPI YA FEDHA

## 3.2 **Kuwasilisha Mizania kwa kifupi (Statement of Financial Positio**

| | 30.06.2015 | 30.06.2014 |
|---|---|---|
| A) Mali za kudumu za muda mrefu (Non-Current Assets). | **Shs** 7,153,818 | **Shs** 10,066,758 |
| B) Mali isiyoshikika (intangible Assets) | 5,260,309 | 8,26,197 |
| C) Rasilimali za muda mfupi (Current Assets) | 531,488,717 | 375,114,668 |
| D) Wadai wa muda mfupi (Current Liabilities) | 2,250,000 | 16,513,166 |
| E) Malimbikizo ya faida (Accumulated Surplus) | 541,652,844 | 376,934,457 |

# ...TAARIFA FUPI YA FEDHA

3.3 **Mtaji wa Mfuko**

| | **30.06.2015** | **30.06.2014** |
|---|---|---|
| ➢ Malimbikizo ya faida | 541,652,844 | 376,934,457 |

3.4 **Kuwasilisha Waraka wa mapato**
(Statement of Comprehensive Income)

| | | |
|---|---|---|
| Faida ya mapato na matumizi | 164,718,387 | 65,848,270 |

3.5 Kuwakilisha Waraka wa Mabadiliko ya Mtaji
(Statement of Changes in Equity)

# ...TAARIFA FUPI YA FEDHA

3.6 Kuwasilisha Waraka wa Mtiririko wa Fedha (Statement of Cash Flows)

| | 2014/2015 TZS | 2013/2014 TZS |
|---|---|---|
| ➢ Fedha zilibaki taslim na Zilizopo benki ni | 404,886,750 | 327,984,067 |

# 4.HITIMISHO

Kwa kuzingatia mawasilisho haya, tunakiomba kikao cha mkutano mkuu wa wadau wa mwaka huu kuazimia yafuatayo:-

1. Mfuko kuendelea kutekeleza malengo ya mwaka 2015/2016 ambayo utekelezaji wake haukukamilika kutokana na changamoto mbalimbali; na
2. Utaratibu wa uchangiaji ulipendekezwa na wadau katika mkutano huu kutumika kwa mwaka 2016/2017 kama utaratibu wa mpito mpaka Serikali itakavyotoa maelekezo kuhusiana na tozo na makato yaliyopo.

# 4.HITIMISHO….

**KAHAWA NI MALI**

**Tuiboreshe – Iwe Bora**

**Tuiongeze – Iwe Nyingi**

**TUTAJIRIKE**

Asanteni kwa kunisikiliza,

Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Kahawa Tanzania,

Andrew P. Kakama

**MWENYEKITI**